

## Hekima ya Shehe

Unapomwambia akitembea sokoni hakuna aliyefikiri kuwa Shehe huyu mzee ni mwenye hekima sana. Akasimama mbele ya duka. Mwenye duka alikuwa akimkaripia kijana aliyekuwa amemkodi kwa ajili ya kumsaidia kutunza vitabu vyake vya hesabu. Sauti yake ilikuwa kubwa kiasi cha kuwafanya watu wengi kusongea karibu na kusikiliza. Ndipo Shehe, mtu mwema na mwenye hekima, akamwambia mwenye duka; "Rafiki yangu, kwa nini unamlaumu kijana huyu? Mwonee huruma, kwa sababu huruma ni tabia ya mtu mkarimu." Mwenye duka akasema: "Bwana, kijana huyu amenijeruhi vibaya sana. Nilipomwajiri aliniambia kuwa anajua kuandika na kutunza hesabu vizuri. Nilimwamini na kumpa jukumu katika biashara yangu. Sasa ninapofungua vitabu vyangu naona hesabu zangu haziko sawa. Hakuna hakika ni kiasi gani tunadai na kiasi gani tunadaiwa."

Isitoshe, wazi kwamba naelekea kufilisika. Shehe akajibu: "Mungu anakuonyesha kwamba mara nyingi vitu vizuri vya dunia hii ni kwa ajili ya wapumbavu, na magumu yake ni kwa ajili ya wenye hekima". Ukifikiri vema juu ya jambo hili, utaona kwamba wewe mwenyewe huko sahihi katika hesabu zako kwa Mungu, sawa na huyu kijana alivyo na hesabu zake kwako. Kadhalika, hujui hivi leo mambo yatakuwaje Siku ya Hukumu, kwamba kutakuwa na faida au hasara. Acha kumkaripia kijana bali ujilaumu mwenyewe, kabla hujasema sana". Shehe alilipokuwa anazungumza, kila mtu alikuwa akimsikiliza kwa makini. Baadaye mtu mmoja akamwambia: "Unasema sawa Shehe. Sasa hebu tuelezee maana ya maneno yako, kwa maana tunaona vigumu kuyaelewa".

Shehe akasema; "Nitawaambia hadithi iliyo na maana nzuri sana." Akaketi kando ya duka akaaza kuzungumza na umati. "Miaka mingi iliyopita," alisema, "kulikuwa na mtu ambaye siku moja alipokuwa peke yake, alihesabu miaka yake. Akagundua kuwa alikuwa na umri wa miaka sitini. Akazihesabu siku akaona kuwa zilikuwa siku 21,000. Akajiambia: "Maskini mwovu mimi. Kama ningefanya dhambi moja kwa siku, dhambi zangu zingekua nyingi ajabu. Naweza kukutana na Bwana wangu na dhambi nyingi hivi!" Kwa aibu, akaanguka chini na kusema; "Nini kitakachotokea ikiwa nitafanya dhambi nyingi kwa siku? Moyo wangu ni mwovu kiasi gani kiasi cha kuwa huru kufanya dhambi bila kujali!" Alihuzunika sana kutokana na moyo wake mwovu na mwingi wa dhambi. Akabaki amelala chini amechoshwa na kutiwa hofu na simanzi.

Shehe alipomaliza hadithi hii ya ajabu, wasikilizaji wake wote wakajifikiria wenyewe na dhambi zao na nini chakufanya dhambi zao zitakapokuwa zimejumlishwa. Mmoja wao akajibu: "Lakini tumefanya matendo mema yanayokabiliana na dhambi zetu." Shehe akajibu akasema: "Bwana, jihadhari, usitegemee mambo mema; ngoja nikuelezee ni nini kilinitokea nilipofikiria kuhusu matendo yangu mema."

"Siku moja," aliendelea kusema, "nilitamani sana kuhesabu makosa yangu na matendo yangu mema. Mwishowe, nikaona kwamba makosa yangu yalikuwa mengi zaidi kuliko matendo yangu mema nikazimia na kuanguka. Nikapatwa na ndoto mbaya. Katika ndoto yangu nilikuwa nimekaa nyumbani na kitabu kimefunuliwa mbele yangu. Kilikuwa kitabu cha matendo yangu na nikaona dhambi upande wa deni langu nikaaza kuhesabu, lakini zilikuwa nyingi mno kiasi cha kushindwa kuhesabu. Katika ukurasa mwingine kulikuwa na matendo yangu mazuri. Haya yalikuwa machache sana na juu yake kulikuwa na maneno makali yameandikwa: "Haki yetu ni taka zinazonuka." Nilipokuwa nikitafakari nikaaza kulia dotoni, nikaamka.

Kisha shehe akasema: "Wapendwa wangu, ndoto niliyokuwa nayo ilikuwa ya kweli. Mmoja wa manabii, Isaya, ndiye alizungumza maneno haya. Ni sawa kwetu sisi sote kuogopa, matendo yetu mema yaonekana si kitu katika Siku ya Hukumu. Lakini nabii huyu, aliyeelezea matendo yetu mema

hakuishia hapo. Katika kitabu chake alizungumzia habari za Mwokozi wa ajabu ambaye Mungu alimtuma kuokoa watu na dhambi zao. Atawafuta watu machozi ya huzuni zao na toba". Mwenye duka akalia: "Mungu na awahurumie wazazi wako! Tuambie nabii alisema nini kuhusu Mwokozi". Shehe akajibu, "Sikiliza kile nabii alichosema. "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa movu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona".

Kwa sababu aliutoa uhai wake hata kufa, akahasabiwa pamoja na hao wakosao. Walakini alichukua dhambi za watu wengi, na kuwaombea wakosaji". Mwenye duka akasema: " Mimi si mwerevu kiasi cha kuelewa maneno haya ,lakini ni matamu kuliko sega la asali. Nakuomba unieleze huyo Mwokozi ni nani ambaye alitoa maisha yake, akafa kwa ajili ya dhambi zetu." "Mpendwa wangu", alisema Shehe, "hebu twende nyumbani kwangu, nami nitakuelezea jambo hili kwa undani zaidi toka katika Kitabu cha Mungu".

Mwenye duka akamwambia yule kijana ambaye alikuwa amemkaripia: "Funga duka sasa na uende kwa amani. Mungu akipenda rudi kesho". Akaondoka na yule Shehe. Walipofika nyumbani kwake, Shehe akaanza kumsomea kutoka vitabu vya manabii na Zaburi (kwa Kiarabu ni Zabur) za Mfalme Daudi (Kwa Kiarabu ni Dawud) nabii. Walisoma unabii kuhusu Mwokozi. Baadaye akamwonyesha Injil ya Yesu, jinsi unabii ulivyotimizwa katika mwanadamu Yesu aliye Masihi. Wote walishangaa juu ya upendo wa Mungu wa ajabu na kufurahia njia ya wokovu.

*Wapendwa, kila mmoja wetu, na afikirie moyo wake ni mwovu na una dhambi kiasi gani. Zihesabu na usithubutu kufikiri kwamba ni chache sana, kwani utajisaliti mwenyewe. Daudi nabii, na mtu aliyempenda Mungu na amri zake, alizihesabu dhambi zake. Aligundua kuwa zilikuwa nyingi akasema: "Maana dhambi zangu zimenifuka kichwa, kama mzigo mzito zimenilemea mno". Usije ukafikiri kwamba dhambi zile ambazo zimefichika kwa wanadamu zimefichika kwa Mungu pia kwa maana hakuna kinachoweza kufichwa kwa Mungu. Sikiliza kile Daudi alichosema kwa ajili ya hili: " Ee Mungu unajua upumbavu wangu, wala wala hukufichwa dhambi zangu". Jichunguze na uje mbele za Mungu na toba. Fikiria maneno haya matakatifu kwa akili na kwa moyo wako wote. Tafuta wokovu wa Mungu, Mwokozi, Bwana Yesu aliye Masihi. Alijitoa akafa kwa ajili ya dhambi zako na kufufuka katika wafu ili na wewe pia uweze kuishi milele.*

*Ili uweze kujifunza zaidi habari za Yesu Masihi na Biblia Takatifu, tuko tayari kukutumia vijitabu vya kukusaidia zaidi. Tafadhali tuma barua yako kwa anwani moja wapo kulingana na mahali unakoishi.*

---

## **Ufafanuzi**

**Kufilisika** maana yake ni kuwa bila fedha au kukosa njia ya kulipa deni.

**Kutunza Vitabu** ni kazi ya utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu.

**Daudi** (kwa Kiarabu ni Dawud) ni Mfalme aliyejulikana sana wa Israeli.

**Takatifu** ni kile kilicho cha Mungu. Vilevile hali na tabia ya Mungu.

**Injil** (Injili) ni neno la Kiarabu lenye maana ya Injili linalopatikana katika maadiko ya Agano Jipya ya Biblia Takatifu.

**Masihi** ni neno la Kiebrania lenye maana ya "Mpakwa mafuta wa Mungu". Alipakwa mafuta kuwa Mwokozi wa watu wote. Neno la Kigiriki la Masihi ni "Kristo".

**Karipia** ni kusema kwa kutumia maneno makali juu ya kosa; kulaumu kwa nguvu. Kemea au adhibu kwa maneno.

**Shehe** ni neno la Kiarabu lenye maana ya mzee, kiogozo wa kabila la Kiarabu au familia. Cheo cha heshima.

**Zabur** ni neno la Kiarabu la kitabu cha Zaburi za Daudi katika Bibilia Takatifu.

- 1) Isaya 64:6
- 2) Isaya 53:1-12
- 3) Isaya 25:8-9
- 4) Isaya 53: 5
- 5) Isaya 53:12
- 6) Zaburi 38:4
- 7) Zaburi 69:5

Kukusaidia kuelewa zaidi kuhusu Yesu Masihi,  
tuko tayari kukutumia vijitabu vingine.

Tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani zifuatazo:

### **HAMASA YA MILELE**

Box 11795 Arusha, Tanzania

Simu: **0767-288053, 0784-288053**

Barua pepe: **hymilele@gmail.com**

### **LIFE CHALLENGE.**

Box 50770, Nairobi, Kenya

Simu: **0728-858.333**

Barua pepe: **coast@lifechallenge.de**